# SOP FOR WARD ROUNDS

**SWR  - SERVICE WARD ROUND**

1. SWR inafanywa kila siku katika kila wodi kwa daktari wa firm kuona wagonjwa wa firm husika.
2. Daktari wa firm atamfahamisha muuguzi wa wodi kwanza na muuguzi wa wodi ataandaa mafaili.
3. Daktari wa firm kabla ya kuanza round ataongea na muuguzi kujua kama kuna mgonjwa anayehiitaji kuonwa kwa haraka ili aonwe mapema na kwa haraka zaidi.
4. Daktari atapita chumba kimoja hadi kingine ili kuwaona wagonjwa wote wa firm yake na ataandika katika faili na chati za tiba.
5. Tiba na maombi yote ya vipimo yataandikwa katika mfumo wa INAYA.
6. Daktari atahakikisha anaweka sahihi katika kitabu cha SWR baada ya kumaliza round.
7. Daktari Bingwa wa zamu atapita kuona wagonjwa siku za mwisho wa wiki na kutia sahihi katika kitabu cha Round siku za mwisho wa wiki na sikukuu.

**MWR – MAJOR WARD ROUND**

1. MWR zitafanywa na jopo la madaktari bingwa wa kila Firm wakiambatana na madaktari wanafunzi na madaktari wa kawaida wa Firm husika kila siku ya Ijumaa.
2. MWR inaweza fanyika katikati ya wiki kutegemea utaratibu wa madaktari bingwa wa firm husika.
3. MWR itaanza kwa jopo la madaktari kukaa pamoja na wauguzi ambao wataandaa mafaili ya wagonjwa. Jopo la  madaktari litahusisha pamoja na wataalamu wengine toka idara mbalimbali ikiwemo taaluma tiba shufaa, madawa, radiolojia na tiba mionzi.
4. Kila maamuzi yatakayofanywa na jopo litakalopita MWR yataandikwa katika jalada la mgonjwa husika na kuingizwa katika mfumo wa INAYA. Daktari bingwa mmoja ataweka sahihi katika kitabu cha MWR cha firm husika baada ya kumaliza round.

**PAR – POST ADMISSION ROUND**

1. PAR itafanywa na daktari bingwa wa firm kwa wagonjwa wa firm yake waliolazwa siku zisizozidi mbili na wasiokuwa na treatment plan kutokana na majibu ya vipimo kuchelewa.
2. Daktari Bingwa atakaepita PAR ataweka sahihi yenye kutambulisha kuwa ni PAR katika kitabu cha SWR cha firm yake.

**ER – EVENING ROUND**

1. ER itafanywa kila siku jioni na daktari bingwa aliyeko zamu kwa wagonjwa wote waliolazwa siku hiyo na hawakuonwa na daktari bingwa.
2. Daktari Bingwa ataandika tiba na maagizo yake katika jalada la mgonjwa na katika mfumo wa INAYA kama kawaida.
3. Daktari aliyepita ER atapaswa kutia sahihi itakayoonyesha kuwa ni ER katika kitabu cha SWR cha firm ya mgonjwa husika.